# Usawiri wa Wanawake katika Vitabu vya Kiada vya Somo la Kiswahili katika Shule za Sekondari Nchini Kenya

Harriet K. Ibala
*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza usawiri wa wanawake katika vitabu vya kiada vya somo la Kiswahili katika shule za secondari nchini Kenya. Matini katika jumla ya vitabu vya kiada 21 yalichanganuliwa. Wilaya ya Kakamega ilitumiwa kama eneo la utafiti ili kukusanya data. Shule 33 zilitumiwa kwa lengo hili ambapo walimu wa Kiswahili 72 na wanafunzi 291 walishiriki katika uchunguzi huu. Nadharia ya kifeministi ya uhakiki wa kazi za kisanaa na ile ya uchanganuzi wa usemi zilitumiwa kuupa utafiti mwelekeo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia programu ya tarakilishi ya SPSS. Uchunguzi huu uligundua kwa jumla kuwa vielelezo vya picha katika vitabu vya kiada viliwasawiri wanaume wengi kuliko wanawake. Vilevile wanaume wengi kuliko wanawake walitajwa. Kama ilivyotarajiwa, wanawake wengi kuliko wanaume walisawiriwa katika majukumu ya kifamilia nyumbani, huku wanaume wakisawiriwa katika ajira za kitaaluma na za hadhi ya juu kuliko wanawake. Maudhui ya vitabu hivi yaliwapendelea wanaume kuliko wanawake. Kutokana na ugunduzi huu, ilipendekezwa kuwa wakuza mitaala wahimizwe kuidhinisha vitabu vya kiada ambavyo vimejumuisha masuala ibuka kama vile jinsia na vilivyosawiri jinsia zote kwa usawa. Aidha, ilipendekezwa kuwa vitabu vitumie mifano ya wanawake waliofaulu na walionawiri katika tasnia mbalimbali kama viigwa bora kwa wanafunzi wa kike. Vilevile wanawake na wanaume wengi wenye mwamko wa kijinsia wajitose katika uwanja wa uandishi ili kuwasawiri wanawake inavyostahiki.**

**Maneno Muhimu:** Wanawake, usawiri, Kiswahili, Shule za Sekondari, Vitabu vya Kiada

## Utangulizi

Suala la usawiri wa wanawake limepewa umuhimu mkubwa kote ulimwenguni. Jambo hili limesisitizwa mno katika tafiti na makongamano ya kimataifa, na hata

katika mifumo ya elimu, hasa shuleni (Davies 1995; UNESCO 1970). Masuala ya kijinsia yameendelea kupata kipaumbile katika sera za kiserikali, hasa katika sekta ya elimu ambapo masuala ya aina hii yamezua hisia na changamoto anuai (Chege na Sifuna 2006). Kutokana na hali hii ulimwenguni, wataalamu na wasomi wa Kiswahili wameshinikiza masuala ya usawa wa kijinsia yajumuishwe katika mitaala ya elimu. Mbali na haya, suala la usawiri wa wanawake katika vitabu vya kiada limepewa msisitizo katika siku za hivi karibuni. Kama wanavyosema Kabira na Masinjila:

> Ni muhimu vitabu vya kiada viwasawiri wanawake kwa njia iliyo sawa. Hii itawezesha wanafunzi wa jinsia zote kutotenganishwa, na kupata maudhui ya vitabu hivi kwa wepesi (1998, uk. 16).

Vitabu hubeba ujumbe muhimu kwa wanafunzi. Kwa hivyo, huwatanabaisha wanafunzi kuhusu usawa wa jinsia. Vitabu vya kiada huyafanikisha haya kupitia mifano ya wanadamu. Pia huonyesha tabia na fikira chanya zinazostahili kufahamika na kuzingatiwa. Taasisi ya Elimu ya Kenya imeandaa jopo maalum la wataalamu wa lugha ya Kiswahili ambalo hukagua vitabu vya kutumiwa katika ufundishaji wa somo hili. Baadhi ya mambo wanayochunguza ni ushahidi wa kujumuishwa kwa suala la jinsia na hasa jinsi wanaume na wanawake wanavyosawiriwa.

Wataalamu mbalimbali waliochangia suala la usawiri wa wasichana na wanawake katika vitabu vya kiada wana misimamo na mitazamo iliyokita kwenye misingi maalum. Obura (1991) kwa mfano alihoji kuwa usawiri mbaya wa wanawake na majukumu yao uliwadunisha wasichana kiasi kwamba hawashiriki kikamilifu masomoni. Mbilinyi (1996) kwa upande wake alidai kuwa vitabu vya kiada huchangia katika kuathiri wasomaji kutokana na maudhui yake. Nao Chege na Sifuna (2006) wakadahili kuwa ni muhimu shule zitumiwe kuwatia motisha wanafunzi wa kike, kupitia vitabu vya kiada ambavyo wao huvisoma kila siku. Uchunguzi huu ulizingatia usawiri wa wanawake katika vitabu vya kiada ili kubaini iwapo somo la Kiswahili linafunzwa kuambatana na mwelekeo wa sasa ulimwenguni ambapo masuala ibuka likiwemo suala la usawa wa kijinsia yamepewa nafasi ya kikati.

Somo la Kiswahili ni la lazima katika shule za umma za sekondari kote nchini Kenya, kufuatana na mahitaji ya mfumo wa elimu wa 8-4-4. Kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili sekondari (Kenya Institute of Education, 2002), somo hili lina wajibu mkubwa wa kupitisha maarifa, stadi, mitazamo, mielekeo na maadili kwa wanafunzi. Vitabu vya kiada ni mojawapo wa malighafi muhimu ambayo hutumiwa darasani, kwani hulipa somo maudhui na uhai (Mbilinyi, 1992; Obura, 1991). Umuhimu wa vitabu unatokana na ukweli kuwa vinaakisi utamaduni. Utamaduni wa mwafrika umempa mwanamke majukumu ya kifamilia ambayo yamemfungia nyumbani. Hali hii imempa mwanamke nafasi ya chini kinyume na

mwanaume. Katika ulimwengu huu wa sasa ulioathirika na mabadiliko na maendeleo ya kielimu, kisayansi na kiteknolojia, ni dhahiri kuwa taasubi hii imepitwa na wakati. Hii ndio maana Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imechukua hatua ya kuwashawishi na kuwahimiza waandishi na wachapishaji wa vitabu vinavyotumiwa katika shule na vyuo nchini kubadilisha hali hii. Tathmini yetu kama walimu wa somo la Kiswahili ya vitabu vya kiada vya awali ni kwamba kijuujuu wanawake wamesawiriwa kwa njia chanya. Lakini uchunguzi wa kina unatambua kuwa wamesawiriwa kwa njia hasi. Inasibu basi maswali yafuatayo yatafutiwe majibu: Je, hali katika vitabu vinavyotumiwa sasa imebadilika? Wizara ya Elimu imefanikiwa kuwazindua waandishi? Haja ya kubainisha hali ilivyo ndiyo iliyochochea utafiti ulioishia kuandikwa kwa Makala haya, kwa kuangazia namna mwanamke alivyosawiriwa, majukumu ya kifamilia waliyopewa wanawake, ajira na matini yanayohusu wanawake katika vitabu vya kiada vya somo la Kiswahili Sekondari.

Makala haya yaliongozwa na nadharia ya kifeministi ya uhakiki wa kazi za kisanaa (Kolodny, 1986) na nadharia ya uchanganuzi wa usemi (Warren, 1981). Kwa kuzingatia nguzo kuu za nadharia hizi, maandishi mbalimbali ya msingi yalipitiwa. Ripoti za elimu za Kenya hasa Ripoti ya Koech (1999:77-78) zimesisitiza haja ya kumtia moyo mtoto wa kike ili ahitimu katika viwango mbalimbali vya elimu. Hivyo basi, mitaala inapasa kutekeleza haya. Bishop (1995) akitilia mkazo umuhimu wa mitaala anasema kuwa mtaala ni jumla ya tajriba zote ambazo mwanafunzi huzipitia akiwa angali shuleni, ambazo hulenga kuleta matokeo yanayotarajiwa katika muktadha wa shule na ulimwengu wa nje.

Mafanikio katika kupitisha maudhui kwenye mitaala hutegemea matumizi ya malighafi ya kufundishia. Aghalabu malighafi haya ya kufundishia huakisi jamii hasa utamaduni wake. Hii ndio maana Mbilinyi (1996) anadahili kwamba vitabu vya kiada vimekuwa wenzo wa msingi unaobeba maarifa, stadi na mielekeo ambayo huwasilishwa kwa wanafunzi. Wanafunzi hawa ni sehemu muhimu ya jamii kwani ndio wanaotarajiwa kuwa wazazi, viongozi na wazalishaji mali sasa na baadaye. Halikadhalika vijana hawa wana jukumu la kujenga jamii mpya iliyoegemezwa kwenye misingi ya usawa.

Vitabu vya kiada, kwa hivyo, ni zana za kikati. Lakini kama anavyosema Obura (1991), usawiri wa kijinsia unaotokea katika vitabu huathiri wanafunzi kwa njia nzuri au mbaya. Kulingana na matarajio ya wengi, elimu inayotolewa itakuwa na manufaa kama maandishi wanayoyasoma wanafunzi yatawakuza kwa njia chanya. Hii ni kwa sababu msichana akiendelea kusoma mambo hasi kumhusu, atakufa moyo katika kazi yake ya darasani. Usawiri wa namna hii ukitiliwa nguvu na msimamo unaomtweza kuchukuliwa na mwalimu kuhusu uwezo wa kitaaluma wa wasichana, huleta matokeo mabaya kwa wanafunzi.

Kwa hivyo, ipo haja ya kuchunguza taswira ambazo hujengwa katika vitabu vya kiada, hasa wakati huu ambapo masuala ya kijinsia yamepewa kipaumbele katika elimu. Kwa sasa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imeidhinisha jopo maalum la Taasisi ya Elimu kuteua vitabu mwafaka vya kutumia katika kufundishia lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari. Jopo hili huchunguza mambo mengi yakiwemo usawa wa kijinsia kwa kutathmini mitazamo, maudhui na namna mada kuhusu wanawake na wanaume zilivyowasilishwa.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu jinsia na vitabu. Utafiti uliofanywa na *'Woman on Words and Images'* (Davies 1995) mwaka wa 1972 kuhusu hadithi 2760 katika vitabu 134 kutoka wachapishaji 14 ulifichua kuwa idadi kubwa ya vitabu vya kusoma vina wahusika wa kiume. Mbali na kubainisha taasubi hii ya kiume, kulikuwa pia na ushahidi kuwa wanaume walijitokeza mara nyingi kama watu werevu, shujaa na wanaomudu mbinu za kupata pesa. Wanawake nao walijitokeza kama watu wanaotegemea wanaume, wanaoonewa, na kukandamizwa. Hebu tutazame sentensi ifuatayo iliyotafsiriwa kutoka utafiti huo: "Jane anatizama John akiunda kidude cha kuchezea." Hapa, Jane amedumazwa. Yaani yeye amesawiriwa kama mtu wa kushuhudia tu. Matokeo kama haya yameungwa mkono na wataalamu wengine kama Davies (1995).

Taasubi hii hudhihirika katika vitabu vya kiada vya viwango vyote vya elimu. Davies (1995) amethibitisha kwamba kuanzia darasa la kwanza hadi la tatu, jumla ya idadi ya ewanawake katika vitabu vya kusoma ilipungua mno, na ubaguzi wa kijinsia ukaongezela. Knopp (1980) katika Davies (1995) alipata matokeo kama haya kule Ujerumani Magharibi katika uchanganuzi wa vitabu vya darasa la kwanza hadi la nne.

Jambo moja la kusikitisha kuhusu upendeleaji wa wanaume katika vitabu vya hadithi za watoto ni kwamba hadithi hizi huwa hazifunzi tu maadili, bali pia huathiri tabia zao. McArthur na Eisen (1976) katika Komoski (1985) wanaonyesha kwamba Watoto wa kiume wa shule za chekechea huchukua muda kufanya kazi fulani kama ishara ya motisha baada ya kusoma au kusikiliza hadithi inayohusu ushindi wa mhusika wa kiume kuliko baada ya kusoma hadithi kama hiyo inayohusu ushindi wa mwanamke.

Ashton (1983), katika Komoski (1985) aligundua kwamba Watoto wa shule za chekechea waliosoma vitabu vyenye picha zinazowasawiri wanaume vyema kuliko wanawake mara nyingi walichagua vidude vya kuchezea vinavyohusishwa na wanaume. Watoto ambao walisoma vitabu ambavyo vilisawiri jinsia zote kwa njia sawa walichagua vidude vya kuchezea vya jinsia zote. Utafiti wa Ashton ulisisitiza kwamba Watoto huathiriwa na kile wanachosoma. Ingawa utafiti wa Ashton ni wa kale kidogo, na unatofautiana na huu wa sasa kiwakati, umekuwa muhimu mno kwa utafiti huu wa sasa kwani swali ni lilelile.

Kwa mujibu wa Mbilinyi (1992; 1996), wanawake wengi kuliko wanaume katika vitabu wamejitokeza katika hali duni. Huenda haya yalitokea hivi kwa sababu waandishi wengi wa wakati huo walikuwa wa kiume. Hata hivyo, katika karne ya ishirini na moja, vitabu vilivyoandikwa na wanawake ni vingi. Licha ya hayo, ukosefu wa wahusika wa kike katika vitabu vya kiada umeongezeka katika shule za msingi, sekondari n ahata vyuo. Basow (1986) anashikilia kwamba ni nadra sana wanawake kutajwa katika vitabu vya kiada kama mashujaa wa kihistoria, viongozi wa serikali au wanasayansi mashuhuri. Banner (1977) anachangia kwamba hata katika vyuo kuna uhaba wa wahusika wa kike katika vitabu vya rejea. Kwa mujibu wa Basow (1986):

> Ukosefu wa wahusika wa kike katika vitabu vya kiada husababisha wasomaji kuchukulia somo kuwa lililohusishwa na zile juhudi za hapo awali za ubabedume. Hali hii hukatisha tamaa ya wanawake kujiingiza katika uwanja unaohusika (uk. 147).

Obura (1991) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa wasichana na wanawake katika vitabu vya kiada vya masomo ya shule za msingi. Obura na wenzake walichanganua jumla ya vitabu ishirini na nne vya masomo mbalimbali katika shule za msingi. Katika vitabu vya somo la lugha ya Kiswahili, Obura alitoa maoni kwamba wanawake wamejitokeza mara nyingi kama mama. Aghalabu wamesawiriwa katika shughuli zisizokuwa za kujipatia mapato. Anatoa maoni kwamba kwa sababu hii wasichana hawafanyi vizuri katika mitihani, kwani wasichana hawaelewi ni kwa nini wawe shuleni ikiwa vitabu vya kiada vya masomo ya Kiswahili na Kiingereza vinasisitiza hali na majukumu ya nyumbani ya wanawake.

Katika utafiti mwingine, Chesaina (1987) aligundua kuwa waandishi wote wanaume na wanawake husawiri mwanamke mwafaka kwa njia chapwa. Katika vitabu vingi mwanamke amepewa majukumu kutokana na malengo ya jamii. Majukumu haya huwa duni na mara nyingi ya kuwatukuza wanaume. Obura (1991) anasema kwamba juhudi za kusawiri wasichana na wavulana kwa njia sawia zinawezekana tu kwa kuwekwa katika nafasi sawa. Anatoa mfano wa kitabu cha shule za msingi ambapo msichana anaonyeshwa akirekebisha gari la mamake, kinyume na matarajio ya kawaida kwamba mwanaume ndio mwenye gari na ndio mekanika. Wamahiu (1998) anapendekeza kuwa ipo haja ya kuandika juu ya wanawake wakenya waliofanikiwa na kuwaweka kama mfano wa kuiga. Haya yanawezekana kupitia uchapishaji wa vitabu vya kiada ambavyo vinasawiri wanawake wanaotajika, wenye asili na tajriba mbalimbali.

Matokeo katika tafiti mbalimbali yameonyesha kuwa wanawake walisawiriwa kama wanaofanya kazi za nyumbani, karani, upishi, ufundi wa kushona nguo na upokezi wa wageni. Wanaume walisawiriwa kama wahandisi, mameneja wa viwanda, marubani, waendeshaji gari la moshi, wakaguzi wa

mizani na vipimo na wahazigi. Ingawa mada ya utafiti huu wa sasa sio ya kisayansi, wajibu wa vitabu vya kiada katika kujenga taswira za hadhi na kiwango cha kushiriki na wajibu wa wanawake katika jamii ni muhimu.

**Data**

Data iliyotumiwa katika uandalizi wa Makala haya ilipatikana kwa kupitia uchanganuzi wa matini, hojaji ya walimu na hojaji ya wanafunzi kukusanya data. Vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu jinsi vilivyoorodheshwa katika kitabu cha manjano (Orange Book) mwaka 2007 viliteuliwa. Majedwali yaliyobeba data kuhusu utokeaji wa vielelezo vya picha na uradidi wa utokeaji wa wanaume na wanawake, majukumu ya kifamilia ya wanaume na wanawake, ajira walizopewa wanawake na wanaume na maudhui yote yanayohusu wanawake na wanaume katika vitabu vya kiada yalitumiwa. Hatua hii ilifanywa kwa kuzingatia matokeo yaliyogawanywa ifuatavyo:

(a) Utokeaji wa vielelezo vya picha na uradidi wa utokeaji wa wanaume na wanawake.
(b) Majukumu ya kifamilia ya wanaume na wanawake.
(c) Ajira waliyopewa wanaume na wanawake.
(d) Maudhui yote yaliyohusu wanawake na wanaume.

Mwongozo huu ulimwezesha kupangwa kwa data kwa uratibu wenye mantiki. Mwongozo huu uliofanyiwa majaribio wilayani Kakamega ili kuhakikisha uhalali na uaminifu, ulisaidia katika kupanga data za kitarakimu kimfumo. Kuhusu data za kimaelezo, hojaji za walimu na wanafunzi zilitumiwa. Wilaya ya Kakamega ina jumla ya walimu 235 wa Kiswahili wa shule za sekondari. Asilimia 30 ya walimu hawa walihusishwa katika uchunguzi huu. Wilaya hii vilevile ina wanafunzi wa sekondari 25719. Baadhi yao walitumiwa katika uchunguzi huu, kimakusudi. Hojaji zilipelekwa shuleni na mtafiti akakubaliana na walimu wa Kiswahili siku ya kuzichukua baada ya kujazwa. Jumla ya walimu 72 na wanafunzi 219 walijaza hojaji. Data kutoka hojaji hizi iliainishwa kutegemea dhamira.

Chanzo kikuu cha data katika uchunguzi huu kilikuwa vitabu vya kiada vya kufundisha somo la Kiswahili vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu kutumiwa katika shule za sekondari nchini Kenya. Idadi ya vitabu hivi ni ishirini na moja, na orodha hii inapatikana katika *Orange book* kilichochapishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Kenya mwaka 2007. Data ya ziada ilitokana na walimu na wanafunzi. Hawa hutumia vitabu hivi katika shughuli zao za siku za ufundishaji na ujifunzaji. Kwa hivyo, waliaminiwa kuwa katika nafasi nzuri ya kuongezea data muhimu kupitia kifaa cha hijaji. Sehemu ya kijiografia ya Kakamega iliteuliwa kama eneo la utafiti kwa sababu hii.

## Matokeo

### Utokeaji wa Wanawake na Wanaume katika vielelezo vya Picha

Katika uchanganuzi wa matini ya vitabu vya kiada, kidato cha kwanza hadi cha nne, 33% ya vielelezo vya picha vilivyosawiriwa ni vya wanawake ilhali 67% ni vya wanaume. Matokeo haya yanaonyesha kwamba kwa kila vielelezo viwili vya wanaume vinavyosawiriwa kimoja cha mwanamke hutokea.

Maoni ya wanafunzi hayakutofautiana kwa kiwango kikubwa na matokeo ya uchanganuzi wa matini wa vitabu vya kiada. Kutokana na uchanganuzi huu, 72% ya wanafunzi walikuwa na maoni kwamba vielelezo vya picha vya wanaume ni vingi kuliko vya wanawake na 28% wakawa na maoni kwamba vielelezo vya wanawake ni vingi.

Maoni ya 74% ya walimu kutokana na hojaji ni kwamba vielelezo vya picha vya wanaume ni vingi, ilhali 26% yao walikuwa na maoni kwamba vielelezo vya picha vya wanawake ni vingi. Ilitarajiwa kwamba maoni ya walimu yangekuwa sambamba na uchanganuzi wa matini wa vitabu vya kiada.

### Utokeaji wa Wanawake na Wanaume

Kutokana na muhtasari wa utokeaji wa kijinsia, wengi wa wanawake waliosawiriwa katika vitabu vya kiada walihusishwa na majukumu ya kifamilia na masuala ya utetetezi wa haki za wanawake.

Wanaume wengi zaidi ya wanawake walisawiriwa kuhusika na utoaji wa uamuzi, adhabu katika kazi za kiofisi na uhuru wa kijinsia. Ipo haja ya kusawiri idadi kubwa ya wanawake katika makundi haya katika vitabu vya kiada kama mojawapo ya mbinu ya kuleta mwelekeo mpya wa kijinsia kwa msingi wa usawa na uwiano.

### Majukumu ya Kifamilia

Majukumu ya kifamilia ambayo wanaume wamepewa katika vitabu vilivyofanyiwa uchunguzi kwa jumla ni mapishi, kulima, kuchunga mifugo na kukimu jamii. Majukumu waliyopewa wanawake ni ulezi wa watoto, usafi, kwenda mtoni, kutafuta kuni, mapishi na kwenda sokoni.

Ni bayana kwamba jukumu la kulima, kutokana na vitabu vilivyofanyiwa uchunguzi, si la jinsia zote bali ni la jinsia ya kiume. Jukumu la mapishi lilijitokeza wazi kama jukumu la jinsia zote mbili kutokana na muhtasari wa vitabu vyote ishirini na moja vilivyofanyiwa uchunguzi.

### Ajira

Muhtasari wa uchanganuzi wa vitabu kuhusu ugawaji wa ajira kijinsia ulionyesha kwamba ajira walizopewa wanaume kwa wingi katika vitabu vya kiada ni kiongozi, mkurugenzi/meneja, mwalimu na ajira zilizoelezwa mwanzoni kama

ajira za jinsia zote. Ajira walizopewa wanawake ni kiongozi, mkurugenzi/meneja, mwalimu, ajira za jinsia zote na karani au mshauri.

Hata hivyo ilithibitisha kutokana na uchunguzi huu kwamba 71% ya waliosawiriwa katika ajira ni wanaume na 29% ni wanawake. Usawiri huu unabainisha kwamba wanaume wengi kuliko wanawake wamesawiriwa katika ajira hasa za kitaaluma.

Uchanganuzi wa msururu wa vitabu vya kiada vinavyotumiwa kufundishia Kiswahili shule za sekondari umebainisha kuwa hakuna mwanamke aliyepewa jukumu la hamali. Ajira walizopewa wanawake kulingana na maoni ya wanafunzi ni zile ajira za kitamaduni walizokuwa wakifanya wanawake tangu jadi. Kutokana na maoni ya walimu, ni wazi kwamba vitabu vya kiada havijasawiri wanawake katika ajira za kisasa.

**Mwelekeo wa Matini Kijinsia**

Ilitokea kuwa 33.5% ya jumla ya maudhui ya kijinsia katika vitabu vya kiada 21 vilivyofanyiwa uchunguzi yalirejelea ukombozi wa wanawake. Huu ni mwelekeo ambao unathibitisha kwamba ni wakati ambapo haki za kijinsia zinafaa zitekelezwe kwa kiwango wastani.

Unyama dhidi ya wanawake na taasubi ya kiume vilevile yamejitokeza kwa kiwango wastani kama baadhi ya maudhui makuu ya kijinsia katika vitabu vya kiada.

Maudhui ya hatua za kisheria dhidi ya wanawake hayajapewa umuhimu unaostahili na ilhali ndio mwanzo wa ukombozi kamili katika jamii.

Aidha maudhui ya kubaguliwa kwa wasichana katika kiwango cha familia na watoto wa kike kuozwa kama wangali na umri mdogo, au kupachikwa mimba kama wangali shuleni yalipewa uzito katika vitabu vya kiada.

Matokeo ya uchunguzi huu yanaafikiana na yale ya utafiti wa Obura (1991), Mbilinyi (1992; 1996), na Wamahiu (1998) kuwa wanaume hujitokeza zaidi katika vitabu vya kiada kuwaliko wanawake. Aidha imedhihirika kuwa wanaume hujitokeza zaidi katika kazi za kifahari na za hadhi, wanawake huhusishwa kwa wingi na kazi za nyumbani. Lakini inapohusu kazi za upishi katika hoteli kama taaluma, wanaume ndio huhusika.

**Hitimisho**

Makala haya yanadhihirisha kuwa vitabu vya kiada vimependelea jinsia ya kiume kuliko ya kike katika madhumuni yote matano ya utafiti. Kutokana na maandishi na machapisho yaliyopitiwa kuhusiana na mada hii, data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu na kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wenyewe, mapendekezo yafuatayo yalitolewa:

Wanawake wengi wameshauriwa kuandika vitabu vya kiada ili washughulikie suala la usawiri wa wanawake wenzao kwa njia chanya zaidi. Huenda hali hii italeta mabadiliko na mwelekeo wa waandishi kuupa ukati suala la usawa wa kijinsia.

Wanafunzi wa kike wanahitaji kuzingatishwa mifano ya wanawake waliofaulu na kunawiri katika tasnia mbalimbali maishani. Kwa hivyo itakuwa muhimu kwa taarifa za ufahamu, ufupisho na hata mifano ya sentensi katika matini kutumia wanawake hawa wanaotajika, ili wanafunzi wa kike wapate msukumo wa kujikakamua kielimu. Wakuza mitaala waandae mikakati kabambe ya ufundishaji itakayowezesha utatuzi wa matatizo ya usawiri wa kijinsia katika mitaala ya somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Kenya. Hii ni pamoja na kuwapa walimu mwamko kuhusu umuhimu wa usawa wa kijinsia na nyenzo za kufundishia zinazoakisi usawa kijinsia. Jopo la kuteua vitabu vya kiada lizingatie suala la kijinsia katika vitabu kisawasawa kabla ya kuviidhinisha. Pamoja na haya, jopo lifanye juhudi za makusudi za kuwazindua waandishi na wachapishaji kuhusu usawa wa kijinsia.

Ingawa matokeo ya uchunguzi huu yametoa mwanga kiasi, pana haja ya kutafitia mambo yafuatayo:

(a) Usawiri wa wanawake na wanaume katika vitabu vya kiada vya viwango vingine vya elimu nchini, kama vile shule za msingi, za chekechea na vyuo vikuu.

(b) Athari ya maudhui yanayopendelea jinsia ya kiume katika vitabu vya kiada vinavyotumiwa kufundishia somo la Kiswahili katika shule za sekondari, kwa wanafunzi.

(c) Ufundishaji wa masuala ya kijinsia katika shule za sekondari.

(d) Mtazamo wa waandishi wa vitabu vya kiada vya somo la Kiswahili kuhusu masuala ya kijinsia.

## Marejeleo

Basow, S. (1986). Gender Stereotypes, Traditions and Alternatives. Cole Publishing Company, California.

Bishop, G. (1985). Curriculum Development: A Textbook fir Students. London: Macmillan Education.

Chege, F. & D. Sifuna (2006). Girls and Women's in Kenya: Gender Perspectives and Trends. UNESCO, Nairobi.

Chesaina, C. (1987). Women in African Drama: Representations and Role. Unpublished Ph.D Thesis. Leeds University, UK.

Davies, B. (1984). Gender Bias in School Textbooks. Commonwealth Secretariat, London.

Fawe News (1998). The News Magazine of Girls and Women in Africa Volume 6 No.3. FAWE, Nairobi.

Kabira, W. W. & M. Masinjila (1997). ABC of Gender Analysis. FAWE, Nairobi.

Kenya Institute of Education (KIE) (2002). Secondary Schools Kiswahili Syllabus. KIE, Nairobi.

Kolodny, A. (1986). "Dancing through the Minefield: Some Observations of the Theory, Practice and Politics of the Feminist Literacy Criticism": In Adams H. & Searle L. (ed). Critical Theory since 1965. University Press of Florida, Tallahasse.

Komoski, P. (1985). Instructional Materials will not Improve until We Change the System of Educational Leadership. P 42, 31-37

Mbilinyi, D. A. S. (1992). "Gender and School Curriculum". Paper Presented at a Workshop on Women in the Publishing World. Dar es Salaam.

Mbilinyi, D. A. S. (1996). Women and Gender Relations in School Textbooks, Gender Relations and Women's Images in Media. Dar es Salaam University Press, pp 91, Dar es Salaam.

Obura, A. (1991). Changing Images: Portrayal of Girls and Women in Kenyan Textbooks. ACTS Press, Nairobi.

Republic of Kenya, (2006). Approved List of Primary and Secondary Schools Textbooks and Other Instructional Materials. Ministry of Education, Nairobi.

Republic of Kenya, (1999). Report of the Commission of Inquiry into the Education System of Kenya (Koech Report) Government Printers, Nairobi.

UNESCO (1990). Conference on Education for All: World Declaration of Education for All and Framework for Action to Meet Basic Learning Needs. Tomtien (mimeograph)

Wamahiu, S. (1998). Continuity Change in Adoga Women's Roles Status and Education: An Exploratory Anthropological Study. Unpublished Ph. D Thesis. Kenyatta University, Nairobi.

Warren, C. (1981). "Adopting Textbooks" in Cole J. & Sticht T. (eds). The Textbook in American Society, Washington D. C. Library of Congress.